

Utaratibu unaendelea kupitiwa na kurekebisha. Kwa toleo la hivi karibuni, tafadhali tembelea <https://salkeiz.sharepoint.com/qam/SitePages/Home.aspx>

1.0 UPANA:

- 1.1 Wanafunzi, wafanyakazi na wageni wa wilaya wataweza kupatiwa vifaa vya shule maalumu kwa jinsia yao kulingana na utambulisho wa jinsia yao. Upatikanaji wa vifaa vya kibinafsi kulingana na usiri, usalama au wasiwasi mwingine pia.

2.0 MAANA:

- 2.1 **Utambulisho wa Jinsia:** Mtu binafsi kujitambua jinsia kwa undani ambapo inajumuisha kuwa mwanamke, mwanaume, jinsia nyingine, jinsia mbalimbali au huna jinsia.
- 2.2 **Kutokuwa na jinsia:** Mahali au shughuli ambazo zinafikiwa na jinsia zote.
- 2.3 **Jinsia maalumu:** Mahali au shughuli ambayo inafikiwa kwa watu wajinsia moja (kama vile wanawake au wanaume)

3.0 UTARATIBU:

- 3.1 Wanafunzi, wafanyakazi na wageni wataweza kutumia vyoo kulingana na jinsia ya utambulisho wao. Kama vitakuwepo, wale wasiokuwa na jinsia wanaweza kutumia vyoo ambavyo havina jinsia yeyote na yule anayependa usiri,
 - 3.1.1 Shule zinatakiwa kuchukua hatua kuhakikisha vyoo visivyo na jinsia vinapatikana kwa wanafunzi, wafanyakazi na wageni. Vyoo vilivyopo na vinavyotumika na mtu mmoja vinaweza kubadilishwa na kuwa vyoo visivyokuwa na jinsia ili kuweza kutumika kupitia Maombi ya Mchakato wa Marekebisha ya Maeneo kama yanavyooneshwa kwenye [FAC-P020](#) (Vifaa: Maombi ya Huduma). Vyoo vilivyobadilishwa vinatakiwa kuwa nje ya korido kubwa au nafasi rahisi kuweza kufikiwa bila kuomba rufusa, kuhitaji funguo au inabidi kwenda kupitia nafasi ambayo inaweza kuwa inatumika (kama vile siyo nje ya ofisi). Kama hakuna chaguzi za kuweza kubadilisha, angalia ambayo ni karibu na kuweza kufikiwa na wengi katika shule. Shule zinatakiwa kutoa kipaumbele kwa kufuata Sheria ya Ulemavu ya Amerika katika mchakato wa kuchagua
 - 3.1.2 Vyoo ambavyo vitabadilishwa kuwa vya jinsia zote vitawekea alama mlangoni, vitasa vitabadilishwa na kuwa wazi wakati wote labda tu wakati vinatumika, kutakuwa na vitu vya usafi na vyombo vya kutupia uchafu.
 - 3.1.3 Hakuna mtu atakayetakiwa kutumia choo kisichoendana na jinsia ya utambulisho wake.
- 3.2 Wanafunzi wanaweza kutumia chumba cha kubadilishia nguo kinachoendana na jinsia ya utambulisho wao. Huko kwenye chumba kama itahitajika kubadilisha nguo mbele ya watu wengine, wanafunzi watakaotaka kutumia chumba hicho kulingana na jinsia ya utambulisho wao wataweza kufikiwa kupatiwa nafasi ya kuelezea wasiwasi wa usiri. Hiyo nafasi inaweza kuwa, lakini sio hiyo tu:
 - 3.2.1 Kutumia eneo binafsi (mfano; choo chenye mlango, eneo linatenganishwa na pazia, ofisi ya mwalimu wa mazoezi) Kama eneo binafsi halipatikani kwenye chumba cha kubadilishia nguo, shule hainabudi kuomba kufanya tathmini ya kuangalia kama eneo la siri linaweza kutengenezwa kupitia kutumia vyoo, mapazia au vigezo vingine vya kutengeneza usiri kwa kutumia Maombi ya Mchakato wa Marekebisha wa Maeneo in [FAC-P020](#) (Vifaa: Maombi ya Huduma).
 - 3.2.2 Ratiba tofauti ya kubadilisha nguo (mfano kutumia chumba cha kubadilishia nguo ambacho kinaendana na jinsia ya utambulisho kabla au baada ya wanafunzi).
 - 3.2.3 Kutumia eneo la binafsi (mfano; kama choo kilicho karibu, ofisi ya afya)
 - 3.2.4 Nafasi inatakiwa kutolewa kama njia ya kulinda usiri wa mwanafunzi wakati huo kukuza utangamano wa kijamii na wanafunzi na fursa sawa ya kushiriki masomo ya viungo na michezo, kuhakikisha usalama na faraja na kupunguza unyanyapaa.



UTARATIBU

Upatikanaji wa Vifaa kwa Wanafunzi na Wafanyakazi wote FAC-P022

3.2.5 Hakuna mtu atakayetumia chumba cha kubadilisha nguo ambacho hakikubaliani na jinsia ya utambulisho wake.

3.3 Vipimo vya elimu ya wilaya kwa ajili ya ujenzi mpya na ukarabati mkubwa ambapo vyoo au vyumba vya kubadilishia nguo viko katika wigo wa kujumuisha ujenzi usio na jinsia, maeneo yenye kukubalika na Sheria ya Ulemavu ya Amerika uwingi na mahali inayoendana na ukubwa wa eneo na idadi ya wanafunzi.

4.0 HATI ZINAZOENDANA:

4.1 INS-A040- Waliobadili jinsia, Wasio na Jinsia, na Wanafunzi Wasiozingatia Jinsia

4.2 Mpango wa Mwanafunzi wa Mpito

4.3 FAC-P020- Kufanyiwa Marekebisho na Maombi ya Kurekebishwa

5.0 KUPITIWA HISTORIA:

Tarehe	Maelezo
2/15/22	Utaratibu Mpya

6.0 KIBALI CHA MAMLAKA:

6.1 Director of Facilities